

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA THELATHINI NA MOJA

26 MEI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA


KIKAO CHA THELATHINI NA MOJA – TAREHE 26 MEI, 2022

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.



MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

IV. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**268. MHESHIMIWA JOSEPHAT SINKAMBA
KANDEGE (KALAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Watumishi wa Kada ya Afya Wilayani Kalambo kwa kuzingatia upungufu uliopo.

**269. MHESHIMIWA REHEMA JUMA MIGILLA
(ULYANKULU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itajenga Shule za Sekondari katika Kata za Sasu, Nhwande, Makingi na Kanonge katika Jimbo la Ulyankulu.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

270. MHESHIMIWA DEODATUS PHILIP MWANYIKA (NJOMBE MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, ni lini Serikali itarekebisha Sheria ya Utakatishaji Fedha inayozuia dhamana kwa Watuhumiwa hata kwa makosa ya kawaida.

WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:

271. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua changamoto za Viwanda vya nguo nchini kwani ni Viwanda 3 tu kati ya 33 vinafanya kazi.

WIZARA YA KILIMO:


272. MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA (NANYAMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Mradi wa Umwagiliaji wa Kijiji cha Arusha chini utatengewa fedha ili uanze kutekelezwa.



V. MAAZIMIO YA BUNGE:



Azimio la Bunge la Kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa miongoni mwa Viongozi wenye ushawishi mkubwa Duniani na kupewa Tuzo ya Mafanikio ya Ujenzi wa Miundombinu


VI. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO
YA MAKAZI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.



**DODOMA
26 MEI, 2022**



**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**